

# WAIPELEKA ROHO YAKO

Na. EMMANUEL SISTI VALERI (E.S.V)

BMMK K/NYEMBE MOROGORO

0714-800745/0782-518744

- 1. *Ee nafsi yangu umhimidi Bwana,  
Wewe,Bwana ,Mungu wangu, Umejifanya mkuu sana;***
- 2. *Ee bwana, jinsi yalivyo mengi matendo yako!  
Dunia imejaa mali zako.***
- 3. *Waiondoa pumzi yao, wanakufa,  
Na kuyarudia mavumbi yao,***
- 4. *Waipeleka roho yako, wanaumbwa,  
Nawe waufanya upya uso wa nchi. (K)***
- 5. *Utukufu wa Bwana na udumu milele;  
Bwana na ayafurahie matendo yake.***
- 6. *Kutafakari kwangu na kuwe kutamu kwake;  
Mimi nitamfurahia Bwana.***